BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**Kikao cha Nne – Tarehe 17 Februari, 2025.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2024/2025.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

41. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Kwa kiasi gani suala la utoaji wa leseni za biashara ndogo ndogo kwa wageni linadhibitiwa ili kuwawezesha wazawa kunufaika na fursa hizi.

146. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwa na utaratibu wa kukusanya taka ngumu katika Halmashauri zetu ambapo wananchi wanalipia ada au tozo.

(a) Je, ni njia gani zinazotumika katika suala zima la kukusanya ada au tozo za taka ngumu kupitia Halmashauri zetu.

(b) Ni lini Serikali itajenga vizimba vya kukusanyia taka ngumu katika eneo la 'Tunguu Site Plan' ambao ni mji mpya katika makaazi ya watu.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

28. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa kuwa moja ya mila na hulka za utamaduni ni ukarimu.

Je, kuna taratibu zozote za kufanyika kwa vitumbuizi kwa wageni wanaokuja kutalii nchini kwetu, vinavyoashiria kufurahia ujio wao hapa nchini kwetu.

30. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa kiasi gani miundombinu mipya ya ujenzi wa barabara katika maeneo mbali mbali inachochea ukuaji wa huduma na sekta ya utalii kwa ujumla.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

87. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kumekuwa na malalamiko ya wakulima hasa wa mboga mboga kuhudumiwa na Maafisa Kilimo wasiokuwa na ujuzi

wa kutosha. Jambo hili linachangiwa na maafisa hao kukosa mafunzo ya kutosha ya vitendo wanapokuwa vyuoni, hali inayowapelekea kushindwa kuwatatulia wakulima changamoto zao.

Je, ni upi mkakati wa Wizara yako kupitia vyuo vyake vya kilimo katika kuwaimarisha Maafisa Kilimo kwa kuwapa elimu ya vitendo ili waweze kuwa na ujuzi wa kutosha wa kuwahudumia wakulima kwa ufanisi.

165. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Tathmini inaonesha uwepo wa tatizo la udumavu wa mifugo yetu wakiwemo mbuzi, ng’ombe, kuku na bata.

(a) Nini chanzo cha tatizo hili.

(b) Ni mikakati gani Wizara yako imechukua kupitia wataalamu wake ili kuwasaidia wafugaji.

**<u>Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:</u>**

21. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Je, sekta ya viwanda inachangia asilimia ngapi ya pato la taifa pamoja na ajira hususani kwa vijana na kinamama.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

54. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kutoa tunzo mbali mbali kwa kazi na matukio ya kiutamaduni, kunaweza kusaidia kutoa hamasa ya kuuendeleza utamaduni wetu.

Je, Wizara kwa kiasi gani inalipa mazingatio jambo hili.

57. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

(a) Ni tafiti ngapi na zipi zimefanyika katika masuala ya mila, silka, desturi na utamaduni wetu.

(b) Ni tafiti zipi kati ya hizo zimeleta matokeo chanya kwa maslahi ya taifa letu.

**<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>**

13. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Wananchi wa kijiji cha Kidundo Mtambwe Kaskazini, wamechukua juhudi ya kujenga skuli ya maandalizi kwa ajili ya watoto ambao hutembea masafa marefu kufuata huduma ya elimu. Pamoja na juhudi hiyo bado wamekwama kuendelea na ujenzi kutokana na hali duni za wananchi hawa.

(a) Je, Serikali imechukua hatua zipi kusaidia hili.

(b) Kwa kuwa jambo hili ni la muda mrefu, ni lini Serikali itawafikiria wananchi hawa kuwamalizia skuli hii ya maandalizi.

114. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na idadi ndogo ya watoto kuandikishwa katika ngazi ya elimu ya msingi ya maandalizi kwa mwaka 2024/2025 hususani kwa Wilaya ya Mjini.

Je, ni upi Mpango Mkakati wa Serikali wa kuondoa changamoto hii.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

110. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa namna gani uwepo wa bandari kavu umesaidia kupunguza kadhia ya msongamano wa makontena kutoka katika Bandari ya Malindi.

**Wizara ya Afya:**

7. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kuna uhitaji mkubwa kwa Hospitali ya Chukwani kutoa huduma ya masaa 24. Pamoja na hilo, kuna changamoto ya vitendea kazi muhimu katika kutoa huduma ya afya kwa wananchi wa jimbo la Kiembesamaki na majimbo jirani.

Kwa kiwango gani Wizara yako inalitambua tatizo hilo na lini italipatia ufumbuzi.

120. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kuna ukweli gani juu ya madai kwamba dawa tembe aina ya Paracetamol [P500] kuwa na virusi vya machupo ambavyo huweza kupelekea kifo kwa mtumiaji.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

50. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Uchumi wa Buluu una umuhimu mkubwa kwa nchi yetu ya Zanzibar.

(a) Ni kilomita ngapi za mraba zinajumuisha eneo la misitu ya mikoko na mwamba wa matumbawe.

(b) Ni kwa kiasi gani uhifadhi wa maeneo haya unatekelezwa ipasavyo.

IV. **HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma, Nam. 11 ya 2016 na Kutunga Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kuweka Masharti Bora ya Kusimamia na Kudhibiti Ununuzi wa Umma na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa Mara ya Pili.

V. **HOJA ZA KAMATI:**

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2024/2025.

Zanzibar, (Raya Issa Msellem)
17 Februari, 2025. **KATIBU WA BARAZA.**